

ST. MARY'S MBEYA SECONDARY SCHOOL
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA KIDATO CHA TATU JULAI
2022 MSIMBO: 021 KISWAHILI

Muda: Saa 2:30

MAELEKEZO:

1. *Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na mbili (12).*
2. *Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali matatu (3) kutoka sehemu C.*
3. *Sehemu A ina alama kumi na tano (15), sehemu B alama arobaini (40) na sehemu C ina alama arobaini na tano (45).*

SEHEMU A (ALAMA 15)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x), kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.

i. Neno “Chawa” lenye maana ya mfuasi au kibaraka wa mtu fulani linaweza kuingizwa kwenye kundi gani la misimu kati ya haya?;

- A. Misimu ya pekee
- B. Misimu ya kihuni
- C. Misimu bandia
- D. Misimu ya kitarafa
- E. Misimu zagao

ii. “Mzee Mitomingi amelewa pombe”. Je, neno Mitomingi katika tungo hii limetumika kama aina gani ya kivumishi?

- A. Kivumishi cha pekee
- B. Kivumishi cha jina kwa jina
- C. Kivumishi cha sifa
- D. Kivumishi cha namna
- E. Kivumishi cha idadi

iii. Mwalimu wa Kiswahili alisikika akifundisha wanafunzi namna ya kufuatisha maneno katika sentensi ili kuleta maana sahihi. Kwa kuzingatia sarufi ya Kiswahili, je, mwalimu alikuwa anafundisha tawi lipi la sarufi kati ya haya?:

- A. Sarufi Matamshi
- B. Sarufi Muundo
- C. Sarufi Maana
- D. Sarufi Maumbo
- E. Sarufi Mofolojia

iv. Mzee Mwakipesile ana watoto watano, wanne kati ya hao wamebatizwa majina kutoka nomino za pekee na mmoja amebatizwa jina kutoka nomino za dhahania. Je, unafikiri mtoto wa mzee Mwakipesile ambaye ana jina kutoka nomino za dhahania atakuwa nani kati ya hawa?;

- A. Januari
- B. Faraja
- C. John
- D. Amosi
- E. Masanja

v. Mkuu wa shule wakati anawashauri wanafunzi waliofanya vibaya mtihani alisema kazeni kamba .Je, mkuu wa shule alitumia kipera gani cha semi kuwasihi wanafunzi wake kuongeza bidii?

- A. Nahau
- B. Methali
- C. Kitendawili
- D. Mizungu
- E. Msemo

vi. Mwajuma ni mvuvi mahiri katika ziwa Nyasa na hupenda kuimba nyimbo za kujiliwaza awapo katika shughuli zake za uvuvi. Je, nyimbo zinazoimbwa katika muktadha huu kifasihi huitwaje?

- A. Kimai
- B. Tendi
- C. Wawe
- D. Kongozi
- E. Nyiso

vii. Wakati wa sherehe za Mei mosi mwaka huu, wafanyakazi walishuhudia ushairi wa malumbano kuhusu ipi ni kazi muhimu kati ya udaktari na ualimu na mwishowe watambaji walikubaliana kuwa kazi zote ni muhimu kwa jamii. Je, unafikiri wafanyakazi walikuwa wanashuhudia kipera gani kati ya hivi?

- A. Maghani
- B. Majigambo
- C. Ngonjera
- D. Tenzi
- E. Tendi

viii. “Ili kamusi iweze kutumika katika utafiti wa chimbuko la lugha ni lazima iwe inafanua asili za maneno” Je, ni msamiati gani katika kamusi hutumika kumaanisha asili ya neno?

- A. Kisawe

- B. Vitawe
- C. Etimolojia
- D. Homonimu
- E. Kibadala

ix. Rukia alipoulizwa swali lililomtaka abainishe dhima tano za viambishi awali,alitoa hoja nne zilizo sahihi na hoja moja isiyosahihi.Ibaini hoja moja ya Rukia ambayo haikuwa sahihi miongoni mwa hizi;

- A. Kudokeza kauli mbalimbali
- B. Kudokeza njeo
- C. Kudokeza nafsi
- D. Kudokeza ukanushi
- E. Kudokeza urejeshi

x. Mhusika Sekai katika riwaya ya Takadini alikataa kuolewa na Manyamombe Kwa sababu.....;

- A. Sekai hakumpenda Manyamombe
- B. Manyamombe alikuwa mzee mno
- C. Hakutaka kutenganishwa na Takadini
- D. Manyamombe alikuwa masikini
- E. Manyamombe alikuwa na wake wengi

| | | | | | | | | | |
|---|----|-----|----|---|----|-----|------|----|---|
| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
| | | | | | | | | | |

To Get a full post, click [here](#) and then find a post in our Group as titled in this post!